



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA
OFISI YA WAZIRI MKUU,
TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA**



Unapojibu Tafadhali Taja:

Kumb.Na KMC/R.30/7/145

14 Mei, 2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA

Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kupitia Wizara ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia wazee na watoto kwa kuzingatia Muongozo wa usimamizi wa maduka ya dawa yanayoendeshwa na vituo vya kutolea huduma za afya kwa umma sambamba na Mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa Wataalamu wa Afya Mkurugenzi wa Manispaa Kahama anapenda kuwatangazia Wanachi wote wenye Sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa Kahama, kuomba nafasi za Mkataba kuanzia tarehe **14 Mei, 2026**.

1.0. MTEKNOLOJIA DARAJA II – RADIOGRAFA (RADIOLOJIA) – NAFASI (02)

1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya kwanza katika Fani ya Sayansi ya Mionzi (X-ray) kutoka katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam au chuo kingine chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTEKNOLOJIA DARAJA II – RADIOGRAFA (RADIOLOJIA)

- Kuwapima wagonjwa wanaolekezwa kwenye eneo lake la kazi
- Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi
- Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (diagnostic quality)
- Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa
- Kusimamia watumishi walio chini yake
- Kutoa Ushauri kuhusu masuala ya na kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.
- Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization)
- Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.

- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA TGHS B1

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali katika ngazi ya **TGHS B1** kwa mwezi na kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa Wataalamu wa Afya kwa waombaji wa nafasi za Mkataba watalipwa nusu Mshahara ya nafasi husika iliyotangazwa.

2.0. MTEKNOLOJIA DARAJA II – (DAWA) NAFASI – (04)

2.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya kwanza katika Fani ya Mteknolojia Dawa (Pharmaceutical Technologist) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiriwa na baraza la Pharmacy na awe na leseni hai.

2.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTEKNOLOJIA DAWA DARAJA II

- Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
- Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi
- Kuchanganya dawa
- Kuhifadhi dawa na vifaa tiba
- Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa
- Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi
- Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.
- Kuratibu kazi za kamati ya dawa ya hospitali
- Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
- Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi
- Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.
- Kusimamia utendaji wa kazi watumishi walio chini yake
- Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

2.0.3 NGAZI YA MSHAHARA TGHS B1

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali katika ngazi ya **TGHS B1** kwa mwezi na kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa Wataalamu wa Afya kwa waombaji wa nafasi za Mkataba watalipwa nusu Mshahara ya nafasi husika iliyotangazwa.

0 **MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.**

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri wa miaka 18 mpaka 45
- ii. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.
- iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.
- v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa
- vi. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- vii. Waombaji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni
- viii. Kwa waombaji wote wa nafasi ya **Mteknolojia Dawa II** mnaelekezwa kuambatisha Leseni iliyohuishwa.
- ix. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza.
- x. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **28 Mei, 2026.**
- xi. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe na kutumwa kwa njia ya Posta au yawasilishwe Ofisi ya Masijala ya wazi kwa;
Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472,
KAHAMA – Shinyanga.
- xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na


Masudi S. Kibetu
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA
KAHAMA